# UMEKUWA MAKAO YETU

## Zab. 90: 3-6, 12-14, 17 (K) 1

**Frt. Anga Anselim**
**Makunganya-Mahenge-2022**

con passione






1. Wamrudisha  mtu mavumbini,
   Usemapo, Rudini, enyi wana**da**mu/
   Maana miaka elfu machoni pako,
   Ni kama siku ya jana ikiisha kupita,
   Na kama kesha **la u**siku.

2. Wawagharikisha, huwa kama usingizi,
   Asubuhi huwa kama majani yame**a**yo/
   Asubuhi yachipua na kumea,
   Jioni yakatika na **kuka**uka

3. Basi, utujulishe kuzihesabu siku zetu,
   Tujipatie moyo wa He**ki**ma/
   Ee Bwana, urudi, hata lini?
   Uwahurumie watu**mishi** wako.

4. Utushibishe asubuhi kwa fadhili zako,
   Nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu **zo**te/
   Na uzuri wa Bwana Mungu wetu, uwe juu yetu,
   Na kazi ya mikono yetu ui**thibi**tishe.

anganselim625@gmail.com